


# “NENO KUJA KUISHI KATI YETU"

Hujambo!

Nakusalimu asubuhi ya leo.

Wiki iliyopita tulimwona Yesu akiwa mwili na pia Neno la Mungu aliyeumba kila kitu (Yohana 1:1-13). Kwa maneno mengine, Neno la milele lilikuja kufanya makao yake ndani ya Yesu wa Nazareti.

Tunaendelea juma hili na Yohana 1:14-18.

**Yohana 1:14** *'Naye Neno akawa mwanadamu, akakaa kwetu. Nasi tumeuona utukufu wake, utukufu wake yeye aliye Mwana wa pekee wa Baba; amejaa neema na ukweli.*

Neno alifanyika mtu - yaani Yesu. Aliishi kati yetu kwa muda. Neno "makao" katika Kigiriki (ἐσκήνωσεν) maana yake "kutandaza hema". Hali hii inamuunganisha Yesu na Hema Takatifu kule jangwani, ambapo uwepo wa Mungu uliishi kati ya Waebrania katika Hema la Kukutania baadaye walipotoka Misri (tizama Kutoka 25-27).

Sasa tunajifunza jambo lingine - Yesu ni zaidi ya uwepo wa Neno la Mungu - yeye ni  Mwana wa Mungu. Na katika Mwana tunaona mambo mawili muhimu: NEEMA YA MUNGU na UKWELI WA MUNGU.

Katika Yesu tunakutana uso kwa uso na NEEMA YA MUNGU: upendo wake, rehema zake na msamaha wake. Katika Yesu pia tunakutana uso kwa uso na UKWELI WA MUNGU: Mungu ni mtakatifu na atahukumu dhambi zote na wenye dhambi wote.

Ili kumhubiri Yesu-aliye ama Yesu Halisi, lazima tuhubiri hali zote mbili za Mungu katika Kristo Yesu: utakatifu na hukumu yake ya haki juu ya dhambi, na hamu yake kubwa ya kutuokoa sisi sote kutoka katika dhambi zetu ili tuishi maisha matakatifu - sasa na hata milele.

**Yohana 1:16-17** *Kutokana na ukamilifu wake sisi sote tumepokea neema kupita neema. Maana Mungu alitoa sheria kwa njia ya Musa, nayo neema na kweli vimetujia kwa njia ya Yesu Kristo*.

Hakuna anayeokolewa kwa kushika Sheria kwa sababu Sheria (iwe sheria ya Kiyahudi, sheria ya Kikristo, sheria ya Kiislamu) haiwezi kumwokoa mtu yeyote. Kama Paulo alivyoandika:

> ***15*** *'Kweli,* ***16*** *sisi kwa asili ni Wayahudi, na si watu wa mataifa mengine wenye dhambi! Lakini, tunajua kwa hakika kwamba mtu hawezi kufanywa mwadilifu kwa kuitii sheria, bali tu kwa kumwamini Yesu Kristo. Na sisi pia tumemwamini Yesu Kristo ili tupate kufanywa waadilifu kwa njia ya imani yetu kwa Kristo, na si kwa kuitii sheria*.’ Wagalatia 2:15-16

Kilele kinakuja na tangazo la kwamba Yesu ni Mungu kamili na mwanadamu kamili:

**Yohana 1:18** 'Hakuna mtu aliyemwona Mungu kamwe. Mwana wa pekee aliye sawa na Mungu ambaye ameungana na Baba, ndiye aliyetujulisha habari za Mungu.’

Kwa hivyo hii ina maana gani kwa watu wa Afrika Mashariki? Kwa ajili yako? Kwa ajili yangu?

> ‘**34** Yule aliyetumwa na Mungu husema maneno ya Mungu, maana Mungu humjalia mtu huyo Roho wake bila kipimo. **35** Baba anampenda Mwana na amemkabidhi vitu vyote.
> **36** Anayemwamini Mwana anao uhai wa milele; asiyemwamini Mwana hatakuwa na uhai wa milele, bali ghadhabu ya Mungu hubaki juu yake.’ Yohana 3:34-36

Nakuuliza:

• Je, huyu ndiye Yesu ambaye umempa maisha yako?

• Je, huyu ndiye Yesu unayempenda na kumtumikia?

• Je, huyu ndiye Yesu unayemhubiria wengine?

Basi ushikilie sana na zaidi. Usiangalie nyuma kamwe. Maliza ulichoanza. Kwa uwezo wa damu ya Kristo na ushuhuda wako, utaushinda ulimwengu, mwili wako, na ibilisi.

Ni hayo kwa sasa. Hii ni milele.

**JUMA LIJAYO**: Tutaangalia mengi kuhusu Yesu-Aliye ama Yesu Halisi, tukitizama Wafilipi 2:5-11.

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.



Douglas Van Devender.
Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.

**TANGAZO LA KUZINGATIA:**
Wengine wanaweza kuongezwa kwenye orodha yetu ya barua-pepe kwa kutuma majina yao, eneo na barua pepe kwa WDV2023@outlook.com
(Mtu yeyote anaweza kujiondoa kwa kutuma neno STOP kwa anwani sawa ya barua pepe.) Ahsante.